

MKATABA WA MAUZIANO NYUMBA.

Mkataba huu umefanyika leo tarehe..... 03 mwezi..... 02 mwaka 2022

KATI YA

SHAHI ENGINEERING AND CONSTRUCTION COMPANY LIMITED, kampuni iliyo sajiliwa Tanzania yenye anuani ya S.L.P 76582 Dar es Saam ambayo hapa itajulikana kama "MNUNUZI" jina hili lifahamike katika sehemu zote atakapotajwa kama MNUNUZI, pia litahusisha watendaji/warithi wake kwa upande mmoja.

NA

HABIBA SHOMARI SAID wa S.L.P..... Dar es Saam ambaye hapa atajulikana kama "MUUZAJI" jina hili katika maandishi haya litahusisha pia watendaji/warithi wake kwa upande mwingine.

KWAMBA Muuzaji alikua mke halali wa marehemu JUMA MWISHEHE aliyekua mmiliki halili wa eneo na nyumba iliyosajiliwa kama Plot No. 431 Block B, House, Street Kiwalani (Kipawa), kata ya Kiwalani, wilaya ya Ilala, Mkoa wa DAR ES SALAAM.

NYUMBA HIYO KATIKA MKATABA HUU IMEPAKANA NA WATU WAFUATAO:-

1. Upande wa Mashariki : Barabara ya Mtaa
2. Upande wa Magharibi :
3. Upande wa Kaskazini: Shahi engineering and Construction Company ltd
4. Upande wa Kusini: Chanzi

MKATABA HUU UNASHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:-

KWAMBA, MUUZAJI kwa hiari yake mwenyewe, akiwa na akili timamu kwa kuafikiana na watoto wake wote ameamua kuuza NYUMBA kama ilivyotajwa katika MKATABA HUU Kwa thamani ya mauzo ya Shilingi za kitanzania Milioni Sitini na Tano tu (TSH 65,000,000/=).

KWAMBA, MNUNUZI kwa hiari yake mwenyewe, akiwa na akili timamu ameamua na kuridhia kununua NYUMBA HIYO kama ilivyotajwa katika MKATABA HUU Kwa thamani iliyotajwa hapo juu.

1. **KWAMBA, MUUZAJI** anaafiki kiwango cha Shilingi za kitanzania Milioni Sitini na Tano tu (Tsh. 65,000,000/=) kama bei ya makubaliano kwa pande zote mbili kuhusiana na thamani ya NYUMBA kama iliyotajwa hapo juu.
2. **KWAMBA**, nyumba hii imesajiliwa kwa jina la marehemu JUMA MWISHEHE aliyefariki mwaka tarehe 12/07/2007, na kwamba baada ya kifo cha marehemu nyumba

H. Shomari

Amici Digi

ilibaki kwa mke wake kama mmiliki baada ya kifo cha mumewe. Kwamba familia ilikaa kikao na kumteua muuzaji kama msimamizi wa mirathi juu ya mali hii na kuamua kuwa nyumba iuzwe na fedha zigawanye kwa warithi. Hivyo basi Muuzaji amekua mmiliki na muangaliziwa kwa kipindi chote baada ya kifo cha mumewe na ameidhinisha na familia kufanya mauziano hay kama msimamizi wa mirathi.

3. **KWAMBA**, Muuzaji na marehemu Juma Mwishehe walikua na watoto sita ambao ndio warithi wao. Na kwamba watoto wote ni watu wazima na wameridhia kuwa mama auze nyumba hii kama ilivyo elezwa katika mkataba huu, na kwamba hawatakua na madai yeyote dhidi ya mali hii.
4. **KWAMBA, MUUZAJI** anathibitisha na kukiri kuwa leo hii tarehe 03/02/2022 Tayari amekwishapokea kutoka kwa **MNUNUZI** jumla ya fedha shilingi za kitanzania Milini Sitini na Tano tu (Tsh. 65,000,000/=) ambapo shilingi Milioni Kumi ililipwa tarehe 13/11/2021 na kiasi cha Million Hamsini na Tano kimekipwa leo wakati wa kusaini mkataba huu na hivyo hakuna deni lolote lililo baki juu ya mauziano ya nyumba hii kama ilivyo kubaliwa katika mkataba huu.
5. Malipo yote yatafanyika kwa njia benki (**Bank Deposit**) kutoka kwa mnunuzi kwenda kwa Muuzaji kupitia Akaunti yake ya benki ya **CRDB Na. 0152619219600** yenye Jina la Akaunti **HABIBA SHOMARI SAID**.
6. **KWAMBA, MUUZAJI** atawajibika kuhakikisha kuwa atatoa ushirikiano na kutenda kwa uharaka ilikukamilisha makubaliano haya na kummilikisha mununuzi nyumba hii kwa masharti kama ilivyo ainishwa katika mkataba huu.
7. **KWAMBA, MUUZAJI** anaahidi na kuthibitisha kuwa ataendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwa **MNUNUZI** endapo atahitajika wakati wowote kuhusiana na jambo lolote linalohusiana na nyumba kwa ajili ya kusaini nyaraka mbalimbali au mchakato mwingine wowote unaohusiana na umiliki wa nyumba kama inavyotajwa katika Mkataba huu.
8. **KWAMBA, MUUZAJI** anakiri na kuthibitisha kuwa kwa kutia saina mkataba huu kwamba Nyumba haina madeni wala mgogoro wa aina yoyote na Mnunuzi pindi atakapo milikishwa nyumba hatabughudhiwa na mtu yeyote.
9. **KWAMBA, MUUZAJI** anathibitisha kuwa ana haki na mamlaka ya kuuza nyumba kama ilivyotajwa hapo juu na kwamba Nyumba haina madeni, haijawekwa rehani au kutolewa kama dhamana, wala haina vikwazo vya aina yoyote.
10. **KWAMBA, MUUZAJI** anathibitisha na kukubali kuwajibika kwa kurudisha fedha iliyotolewa ya manunuzi na fidia ya asilimia Kumi(10) kutoka siku ya mkataba mpaka siku mgogoro ulipo ibuka endapo utatokea mgogoro wa kiumiliki wa eneo la Nyumba